

Na Gretchen Picklesimer Kunney
(Imetokana na hadithi ya kweli)

Hadithi hii imetokea huko Kanada.

Dieter alitaka asikilize mkutano mkuu. Alijaribu kuketi kwa utulivu. Alijaribu kusikiliza hotuba. Lakini kuwa na ulema-vu katika ukuaji kulifanya iwe vigumu kwake kufokasi. Aligaagaa kwenye kochi. Alicheza na wanasesere wake. Alikimbia pande zote.

Kisha alimwalia Baba yake. Baba alikuwa ameketi kwa utulivu na akiwasikiliza wazungumzaji. Dieter naye alitaka kuwa

kama yeye. Kwa hiyo alileta vitu vyake vya sanaa. Pengine kupaka rangi picha kungem-saidia aketi kwa kutulia.

Wakati akipaka rangi, Dieter alimsikiliza Mzee Jeffrey R. Holland akizungumza. Mzee Holland alisimulia hadithi kuhusu Yesu. Yesu alimtaka Kijana tajiri atoe pesa zake zote awape masikini.*

Dieter alitaka kuwasaidia watu ambao pia hawakuwa na pesa za kutosha. Na alipata wazo.

Ni jinsi gani michoro ya Dieter ingeweza kuwasaidia wengine?



Bundi na Nyangumi

“Mama, nataka kupaka rangi picha ya bundi,” Dieter alisema. “Unaweza kuchora moja kwa ajili yangu?”

“Hakika,” Mama alisema. Alimchora bundi. Dieter alichovya brashi yake ndani ya rangi kiasi. Alipaka rangi mabawa ya yule bundi kwanza. Alifanya baadhi ya manyoya kuwa ya kahawia na baadhi ya manyoya rangi ya chungwa. Alipokuwa akipaka rangi, alisikiliza hotuba zingine. Hata wakati hatuba zote zilipo-kuwa zimekwisha, Dieter aliendelea kufanya kazi. Alitaka bundi awe na mwonekano kamili.

Mwishowe Dieter alimaliza. Alimwonyesha Mama bundi yule.

“Anaonekana mzuri sana!” Mama alisema. “Tumtundike juu?”

Dieter alitikisa kichwa chake hapana, “nataka kuiiza na nitoe pesa hizo ili niwasaidie watu wasiokuwa na pesa za kutosha. Kama walivyozungumza hilo katika mkutano mkuu.”

Mama alitabasamu. “Acha tuone nini tuna-weza kufanya.”

Aliituma picha ile iliyopakwa rangi na Dieter mtandaoni ili kuiiza. Mama aliandika kwamba Dieter alisema atatoa pesa hiyo kwenye kituo cha watu wasio na makazi.

Siku iliyofuata, Dieter na Mama walianga-lia tangazo. Dieter hakuweza kuamini! Watu wengi walitaka kununua picha yake. Alifurahi kwamba watu wengi mno walitaka kusaidia.

Mgahawa katika jiji la Dieter uliomba kununua mchoro ule. Walisema wangelipa mara 10 zaidi ya kile Dieter na Mama walichoomba!



Maduka mengine walimwomba michoro pia. Dieter alikuwa na kazi zaidi ya kufanya!


Mama alichora wanyama zaidi na Dieter alileta rangi zake. Alimpaka rangi mbweha, simba na nyangumi. Alimpenda nyangumi zaidi. Alimpa jina “Nyangumi Otis.” Duka la biashara ya vyakula karibu na nyumba yake liliununua. Mara nyingine Dieter alipokwenda kwenye duka, aliiona ikining’inia ukutani!

“Tazama Mama!” Dieter alionesha kwenye mchoro.

“Wao!” Mama alisema. “Sasa wakati wowote tunapokuja hapa, tunaweza kukumbuka jinsi vipaji vyako vilivyowasaidia watu.”

Dieter aliona fahari kwamba watu walipenda michoro yake. Lakini alikuwa na furaha zaidi kwamba aliweza kuwasaidia wengine. Alifurahi kuwa alisikiliza wakati wa mkutano mkuu. ●

* Kutoka “The Greatest Possession,” Liahona, Nov. 2021, 8-10.



Dieter alitengeneza michoro ili auze kwa sababu alitaka kuwasaidia watu. Je, wewe ungewezaje kuwasaidia wengine?